



TAARIFA KWA UMMA

TANGAZO HILI LIMEIDHINISHWA NA MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA)

PROGRAMU YA HATIFUNGANI YA MUDA WA KATI YA BENKI YA AZANIA PLC: TOLEO LA KWANZA - BONDI YANGU



Benki ya Azania inatoa taarifa kwa umma kwamba Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa Programu ya Miaka Mitano ya Hatifungani yenye jumla ya Shilingi 100,000,000,000 (Shilingi za Kitanzania (Tsh) Billioni Mia Moja). Hali kadhalika, CMSA imeidhinisha Toleo la kwanza la Programu ya Hatifungani (Bondi Yangu), lenye jumla ya Tsh Bilioni 30 (ikiwa na uwezo wa kuchukua ziada ya Tsh Bilioni 15), itakayowezesha kupata fedha za kutekeleza miradi yenye malengo ya kimkakati kwenye sekta za uchumi zenye tija.

Taarifa ya Hatifungani Toleo la Kwanza – Bondi Yangu

| | |
|----------------------------------|--|
| Mtoaji: | Azania Bank Plc |
| Jumla ya Kiasi: | TSH 100,000,000,000 (Shillingi za Kitanzania Bilioni Mia Moja) |
| Kiasi cha Toleo ya Kwanza | TSH 30,000,000,000 (Kiasi kitakachozidi kitachukuliwa hadi Tsh 15,000,000,000) |
| Riba iliopangwa (Kuponi): | 12.5% kwa mwaka itakayolipwa mara nne kwa mwaka |
| Kiwango cha chini: | TSH 500,000 (Shillingi za Kitanzania Laki Tano) |
| Tarehe ya Toleo: | 16 Desemba 2024 |
| Tarehe ya Kuiva kwa Hatifungani: | 16 Desemba 2028 |
| Tarehe za Malipo ya Riba: | 16 Machi, 16 Juni, 16 Septemba, 16 Desemba |
| Riba ya Hatifungani: | Asilimia 12.5 kwa mwaka. Riba isiyobadilika itakayolipwa mara nne kwa mwaka |
| Muda wa Hatifungani: | Miaka 4 |
| Kodi: | Hatifungani haina kodi ya zuio |
| Kuorodheshwa DSE: | Hatifungani itaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) |

Uwekezaji unafanyika kwa kujaza Fomu ya Maombi inayopatikana kwenye matawi ya Benki ya Azania; kwa mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam waliopewa leseni na Mamlaka ya Masoko na Dhamana (CMSA); au kwenye tovuti ya Azania www.azaniabank.co.tz

Maombi yatakamilishwa kwa kufanya malipo katika akaunti za benki ya Azania zilizoainishwa hapo chini:

- Akaunti ya Kulipia

| | |
|---------------------------------------|--------------|
| Azania Bondi Yangu Collection Account | 033000001881 |
|---------------------------------------|--------------|

| S/n | Tukio | Tarehe |
|-----|--|-----------------------|
| 1. | Tarehe ya kuidhinishwa kwa hatifungani na CMSA | Alhamisi, 26 Sep 2024 |
| 2. | Tangazo la hatifungani kwa Umma | Jumatatu, 04 Nov 2024 |
| 3. | Kuanza kupokea maombi ya ununuzi wa hatifungani | Jumatatu, 04 Nov 2024 |
| 4. | Mwisho wa kupokea maombi ya ununuzi hatifungani | Ijumaa, 06 Des 2024 |
| 5. | Mgao kwa wawekezaji | Alhamisi, 12 Des 2024 |
| 6. | Kutangaza matokeo ya mauzo ya hatifungani | Ijumaa, 13 Des 2024 |
| 7. | Tarehe ya toleo | Jumatatu, 16 Des 2024 |
| 8. | Kuwasilishwa kwa rejista CSDR | Jumanne, 17 Des 2024 |
| 9. | Kuingiza CDS kwenye mfumo wa DSE | Jumanne, 17 Des 2024 |
| 10. | Kuorodheshwa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) | Jumatano, 15 Jan 2025 |
| 11. | Mwisho wa Hatifungani | Jumatatu, 16 Des 2028 |

Wawekezaji wanashauriwa kuwasiliana na mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wenyе leseni kutoka Mamlaka ya Masoko, Mitaji na Dhamana (CMSA); wahasibu, wanasheria au washauri wengine wa masuala ya fedha kwa ushauri elekezi ili kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

Imetolewa Na:
Mkurugenzi Mkuu,
Azania Bank Plc,
Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
P.O BOX 32089
Dar es Salaam, Tanzania.

Connecting all your banking needs.

customercare@azaniabank.co.tz | 0800 110 210

www.azaniabank.co.tz